JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI MTANDAONI)

## [SHERIA NDOGO]

Toleo hili la Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) za mwaka, 2018, ni Tafsiri Rasmi iliyosanifiwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 84 cha Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sura ya 1.

Dodoma,
..........Oktoba, 2020

ADELARDUS L. KILANGI
*Mwanasheria Mkuu wa Serikali*

TANGAZO LA SERIKALI NA. 913 limetangazwa tarehe 16/10/2020

SHERIA YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 103)*

KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA
(MAUDHUI MTANDAONI) ZA MWAKA 2020

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni Jina*

SEHEMU YA
KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
WAJIBU WA KUWA NA LESENI

4. Leseni.
5. Aina za leseni.
6. Maombi ya leseni.
7. Utoaji wa leseni.
8. Kusitisha na kufuta.

SEHEMU YA TATU
WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI

9. Wajibu wa jumla.
10. Mtoa huduma za maudhui mmiliki wa leseni za wilaya au mkoa.
11. Haki na wajibu wa mwombaji wa leseni za huduma za ziada.
12. Mmiliki wa leseni za habari na matukio mtandaoni.
13. Sehemu ya huduma za intaneti.

SEHEMU YA NNE
MASHARTI YA JUMLA

14. Mtumiaji wa maudhui mtandaoni.
15. Mhodhi maudhui ya mtandaoni.
16. Maudhui yaliyokatazwa.
17. Kutoa taarifa.
18. Kumlinda mtoto.
19. Uwezo wa Mamlaka.
20. Kushughulikia malalamiko.
21. Adhabu.
22. Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 133 la 2018.

MAJEDWALI

SHERIA YA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA,
(SURA YA 306)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 103)*

KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI MTANDAONI), 2020

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) wa Mwaka 2020.

Matumizi

2. Kanuni hizi zitatumika kwa watoa huduma za maudhui mtandaoni, watoa huduma za intaneti, wenye leseni za huduma za ziada, watumiaji wa maudhui mtandaoni na mambo mengine yanayohusiana na maudhui mtandaoni.

Tafsiri

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

Sura ya 306

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta;

Sura ya 172

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mawasiliano Tanzania;

"mmiliki wa leseni za huduma za ziada" maana yake ni mwenye leseni ya Mamlaka katika kundi la leseni za huduma za ziada kwa matumizi pekee ya utoaji wa maudhui mtandaoni au kuwezesha watozi wa maudhui mtandaoni;

"blogu au tovutiblogu" maana yake ni tovuti inayojumuisha uzoefu, mtazamo, maoni ya mwandishi au kikundi cha waandishi ikiwa ni pamoja na habari mpya, matukio, majarida, matangazo na picha, video na miunganiko ya tovuti nyingine;

"mmiliki wa blogu" maana yake ni mwandishi au kikundi cha waandishi kinachomiliki na kuendesha blogu na shughuli nyingine zinazohusiana na blogu;

"maudhui" maana yake ni taarifa kwa njia ya hotuba au sauti nyingine, data, matini au picha ambazo ni mnato au jongevu isipokuwa pale ambapo inarushwa hewani kwa mawasiliano binafsi;

"maudhui yanayohamasisha chuki" maana yake ni maudhui yanayotetea au kuhamasisha mauaji ya kimbari au chuki dhidi ya kundi fulani la watu;

"hotuba za chuki" maana yake ni maelezo yoyote kwa maneno, hotuba, picha, yanayodhalilisha, ya kukashifu au kushusha hadhi ya mtu au kikundi kwa msingi wa mbari, ukabila, dini au ulemavu;

"maudhui ya kudhalilisha" maana yake ni maudhui ya kukwaza, yasiyo ya kimaadili, na kinyume na vigezo na maadili yanayokubalika kama vile maudhui ya utupu na ya ngono;

"sehemu ya kutoa huduma za intaneti" maana yake ni sehemu inayotoa huduma za rejareja ya mtandao, mgahawa au baa au hoteli ndogo isiyo rasmi inayotoa huduma ya mtandao kwa kutumia kompyuta zake au kompyuta za wateja hususan bila malipo;

"mmiliki wa leseni" maana yake ni mtoa huduma mwenye leseni ya Mamlaka katika kundi ambalo linawawezesha watozi wa maudhui mtandaoni;

"chombo cha habari kisichotumia intaneti" maana yake ni vipindi vya redio au televisheni vinavyorushwa hewani na watoa huduma wenye leseni za maudhui mtandaoni kwa kutumia mtandao wa utangazaji wa ardhini;

"maudhui yanayohusiana na habari" maana yake ni taarifa za mtandaoni zilizokusanywa, kujumuishwa, kuhaririwa, kuchapishwa na kutangazwa kwa namna sawa au zile zinazofanana na chombo cha asili cha habari;

"mtandaoni" maana yake ni mazingira ambayo mawasiliano yanapatikana kupitia mtandao ambapo jamii inaweza kupata mtandao ama bila malipo au kwa malipo na ambayo yameanzia au kukusudiwa kutumika Tanzania;

"kihodhi maudhui mtandaoni" maana yake ni seva yoyote inayohodhi au inayoweza kusaidia upatikanaji wa maudhui mtandaoni ambayo inaweza kujumuisha seva za uhamishaji wa faili kiitifaki, seva za simu za intaneti, kampuni za kuhodhi tovuti na seva za tovuti;

"huduma ya maudhui mtandaoni" maana yake ni maudhui yanayotangazwa kwa umma kupitia tovuti za intaneti, programu tumizi za kompyuta, majukwaa, blogu, tovutiblogu, blogu ndogondogo, akaunti ya umma, zana za ujumbe mfupi wa papo hapo, matangazo ya moja kwa moja mtandaoni, mikusanyiko na majukwaa mengine yanayohusiana;

"mtoa maudhui mtandaoni" maana yake ni mtu yeyote anayetoa huduma za maudhui mtandaoni;

"majadiliano ya mtandaoni" maana yake ni mahali pa majadiliano ya mtandaoni ambapo watu wanaweza kujadiliana kwa njia ya kutuma ujumbe au majarida na ambapo majadiliano mengi yanaruhusu watu mbalimbali kuona mijadala iliyotumwa, lakini inahitaji kufungua akaunti ili kutuma ujumbe katika majadiliano ambapo mjadala mpya unaoendelea unatumwa na kujibiwa ndani ya mjadala uliopo;

"jukwaa mtandaoni" maana yake ni kituo cha intaneti ambapo watu wanaweza kupata habari, burudani, elimu, dini au taaarifa nyingine kupitia televisheni, redio, mtandao wa kijamii na blogu za mtandaoni;

"redio mtandaoni, redio tovuti, redio mtandao, redio mtiririko, redio ya kielektroniki, au tovutitangazaji" maana yake ni huduma za kusikika ama zenye leseni au zisizokuwa na leseni ya Mamlaka ambazo zinarushwa kwa njia ya mtandao;

"televisheni mtandao" kwa jina lingine televisheni tovuti ni usambazaji wa maudhui ya televisheni kidijiti, vipindi vifupi au video zilizotengenezwa na kampuni au watu binafsi wenye leseni na wasio na leseni ya Mamlaka ya kutoa huduma kupitia tovuti mkondo ambao inawalenga watumiaji au wananchi wa Jamhuri ya Muungano;

"utangazaji sambamba" maana yake ni utangazaji wa maudhui katika chombo cha habari cha kawaida kupitia jukwaa la mtandao;

"mtandao wa kijamii" maana yake ni huduma za mtandao na majukwaa ambazo zinajengwa katika misingi ya dhana na ya kiteknolojia ya tovuti na kwamba zinaruhusu utengenezaji, ubadilishanaji na muingiliano wa hali ya juu wa watumiaji wa maudhui na majukwaa kupitia watu binafsi, mashirika na jamii kubadilishana, kutengeneza kwa

pamoja, kujadili, na kuboresha maudhui ya watumiaji;

"mtumiaji" maana yake ni mtu au chombo kilichoundwa kisheria kinachopata maudhui ya mtandao ama kwa kujiunga au vinginevyo; na

"ukurasa wa tovuti", "tovuti" au "eneo" maana yake ni majalada ya maudhui yanayopatikana duniani kote kupitia tovuti kwa kuomba URL.

## SEHEMU YA PILI
## WAJIBU WA KUWA NA LESENI

Leseni

4.-(1) Mtu hataruhusiwa kutoa huduma za maudhui mtandaoni bila kupata leseni kutoka Mamlaka.

(2) Mtu ambaye amekiuka masharti ya kanuni ndogo ya (1) anatenda kosa na atakapopatikana na hatia, atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kutumikia kifungo cha miezi kumi na miwili au vyote.

Aina za leseni

5.-(1) Aina za leseni za maudhui mtandaoni zitakuwa kama ifuatavyo:

(a) leseni kwa ajili ya kusimamia maudhui yaliyojikita katika habari na matukio yanayotolewa kwa mtoa huduma za maudhui ya mtandao ambayo maudhui yake yanahusu habari, matukio na matukio ya habari;

(b) leseni kwa ajili ya kutoa maudhui yaliyojikita katika burudani inayotolewa kwa mtoa huduma za maudhui ya mtandao ambayo inajumuisha muziki, filamu, tamthilia mfuatano, tamthilia, drama, futuhi, michezo na maudhui mengine ya burudani yanayohusiana;

(c) leseni kwa ajili ya kutoa maudhui yanayojikita katika elimu na dini inayotolewa kwa mtoa huduma za maudhui ya mtandao ambayo maudhui yake yanahusu taarifa za dini na maudhui yanayolenga kutoa elimu; na

(d) leseni ya utangazaji sambamba inayotolewa kwa mmiliki wa leseni za utangazaji mkondo zenye hadhi ya kitaifa.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1) (a), (b) na (c), "yanayojikita" maana yake ni maudhui ambayo si chini ya asilimia 85 mmiliki wa leseni anayopaswa

kusimamia kulingana na aina ya leseni kwa kiwango kilichopimwa kwa kigezo cha wiki.

(3) Bila kujali masharti ya leseni chini ya kanuni ndogo ya (1) (a), (b) na (c), mmiliki wa leseni atahitajika kutoa maudhui mengine kuhusiana na masuala ya amani ya taifa, usalama wa umma na majanga au dharura.

Maombi ya leseni

6.-(1) Mtu ambaye anataka kutoa huduma za maudhui mtandaoni ataomba kwa Mamlaka kwa kujaza fomu ya maombi kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na atalipa ada kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali la Pili la Kanuni hizi.

(2) Fomu ya maombi itaambatana na-

(a) nakala iliyothibitishwa ya cheti cha uandikishwaji au usajili;
(b) nakala iliyothibitishwa ya Cheti cha Mlipakodi;
(c) nakala iliyothibitishwa ya Cheti Safi cha Kodi kwa kampuni au mashirika yasiyo ya kiserikali;
(d) nakala iliyothibitishwa ya Kitambulisho cha Taifa;
(e) orodha ya mmiliki na timu ya menejimenti;
(f) wasifu wa mfanyakazi;
(g) miongozo ya sera ya uhariri kwa aina ya leseni ya habari na matukio;
(h) maelezo ya kiufundi kwa vifaa vilivyotumika; na
(i) nyaraka nyingine zozote kama Mamlaka itakavyohitaji.

(3) Leseni itakuwa hai kwa kipindi cha miaka mitatu na inaweza kuhuishwa.

Utoaji wa leseni

7.-(1) Mamlaka inaweza kutoa leseni baada ya kuzingatia maombi na kujiridhisha kwamba mwombaji ametimiza masharti yote na amewasilisha maelezo, nyaraka na taarifa nyingine kama itakavyohitajika.

(2) Endapo Mamlaka inakataa kutoa leseni, itamtaarifu mwombaji na kueleza sababu za kukataa pamoja na maelezo mengine yoyote kama Mamlaka itakavyoamua ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kukataa.

Kusitisha na kufuta

8.-(1) Mamlaka inaweza kusitisha au kufuta leseni baada ya kuridhika kuwa vigezo na masharti ya leseni iliyotolewa yamekiukwa.

(2) Kwa kuzingatia kifungu kidogo cha (1),

Mamlaka, baada ya kufuta au kusitisha leseni, itamtaarifu mmiliki wa leseni kwa maandishi ikieleza sababu za kufutwa au kusitishwa.

(3) Endapo leseni imefutwa au imesitishwa, mmiliki wa leseni, baada ya kupatiwa taarifa ya kusitishwa au kufutwa kwa kadri itakavyokuwa, atatakiwa kurejesha leseni kwa Mamlaka ndani ya siku saba.

## SEHEMU YA TATU
## WAJIBU WA MTOA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI

Wajibu wa jumla

9. Mmiliki wa leseni atafuata masharti na vigezo vyote vya leseni na ataangalia yafuatayo:

(a) atahakikisha kwamba maudhui mtandaoni ni salama, hayakikuki masharti ya sheria nyingine zozote;
(b) atazingatia mielekeo na unyeti wa kiutamaduni wa umma kwa ujumla;
(c) ataanzisha sera au mwongozo juu ya matumizi salama ya maudhui mtandaoni na kufanya yapatikane kwa watumiaji wa maudhui mtandaoni;
(d) atatumia zana za kudhibiti kuchuja maudhui yaliyokatazwa;
(e) atakuwa na utaratibu wa kubainisha chanzo cha maudhui;
(f) atachukua hatua za kurekebisha maudhui yaliyopingwa au yaliyokatazwa;
(g) atahakikisha kwamba maudhui yaliyokatazwa kama ilivyoanishwa kwenye Jedwali la Tatu la Kanuni hizi yameondolewa haraka mtandaoni mara baada ya kuamrishwa na Mamlaka;
(h) atawajibika kwa taarifa alizochapisha;
(i) atatumia nywila kulinda vifaa vyovyote vya mtumiaji, vifaa vya ufikiaji au maunzi ngumu kwa kuzuia ufikiaji au matumizi yasiyoruhusiwa na watu wasiotarajiwa;
(j) atalipa ada ya udhibiti;
(k) hatafikia, hatahifadhi, hataweka, hatachapisha, hatasambaza au kutangaza maudhui yaliyokatazwa; na
(l) atashirikiana na maofisa wanaotekeleza sheria katika kutekeleza majukumu chini ya Kanuni

hizi.

Mtoa huduma za maudhui mmiliki wa leseni ya wilaya au mkoa

10. Mtoa huduma yeyote wa maudhui ya chombo cha habari kisichotumia intaneti ambaye ni mmiliki wa leseni ya wilaya au mkoa hatatangaza sambamba maudhui kwa kutumia jukwaa la mtandao.

Haki na wajibu wa mwombaji leseni za huduma za ziada

11.-(1) Mmiliki wa leseni ya huduma za ziada, anapoingia mkataba na wateja, aweke masharti na vigezo vya huduma katika mfumo ambao utakuwa rahisi kufikiwa na watumiaji wake.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mmiliki wa leseni atakuwa na haki ya kukataza au kusitisha upatikanaji wa huduma pale amabapo mtumiaji amekiuka masharti ya Kanuni hizi.

(3) Endapo mmiliki wa leseni ataamriwa na Mamlaka au kujulishwa na mtu aliyeathirika na maudhui au kuwepo kwa maudhui yaliyokatazwa, awajulishe watumiaji wake kuyaondoa maudhui yaliyokatazwa ndani ya saa mbili.

(4) Mmiliki wa leseni atasitisha au kufuta akaunti ya mtumiaji pale ambapo ameshindwa kuondoa maudhui yaliyokatazwa ndani ya saa mbili tangu taarifa ilipotumwa.

Mmiliki wa leseni za habari na matukio mtandaoni

12. Mmiliki wa leseni za habari na matukio mtandaoni atatakiwa-

(a) kuzingatia maadili ya uandishi wa habari, taaluma na masharti ya maudhui ya ndani;
(b) kuwasilisha kwa mdhibiti uthibitisho wa sifa za kitaaluma za mfanyakazi na mpango wa maendeleo ya rasilimali watu; na
(c) kuzingatia umiliki na majukumu ya shirika yaliyotolewa chini ya Sheria.

Sehemu ya huduma za intaneti

13.-(1) Mtu anayeendesha sehemu ya huduma za intaneti atakuwa na wajibu ufuatao-

(a) atahakikisha kwamba kompyuta zote zinazotumika kwa ajili ya intaneti kwa umma katika sehemu inayotoa huduma za intaneti zimepewa anwani ya IP za umma;
(b) ataanzisha na kuchapisha sera ya matumizi salama ya intaneti kwa kuzingatia maudhui mtandaoni na kuiweka sehemu ya uwazi; katika skrini ya kompyuta ya nyumbani au kuiweka

eneo la wazi linaloonekana kwa watumiaji kusoma kabla ya kutumia huduma;

(c) ataweka mfumo wa kuchuja upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa;

(d) ataweka kamera ya ulinzi inayorekodi na kuweka kumbukumbu za shughuli zinazofanyika ndani ya sehemu zinazotoa huduma za intaneti; na

(e) ataweka rejesta mahsusi ya watumiaji wa huduma na kuhakikisha kila mtu anayetumia huduma za intaneti amesajiliwa kwa kuonyesha kitambulisho kinachotambulika.

(2) Picha zilizorekodiwa na kamera ya ulinzi na rejesta ya watumiaji waliorekodiwa kwa mujibu wa kanuni ndogo (1) zitatunzwa kwa kipindi cha miezi kumi na miwili.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA JUMLA

Mtumiaji wa maudhui mtandaoni

14. Kila mtumiaji wa maudhui mtandaoni atawajibika kwa habari atakayotuma kwenye jukwaa la mtandao, chombo cha habari cha kijamii, blogu na vyombo vingine vya habari vinavyohusiana.

Mhodhi maudhui ya mtandaoni

15. Mtu anayehodhi maudhui ya mtandaoni atafuata kanuni za maadili katika kuhodhi maudhui na kuhakikisha kuwa maudhui yaliyotangazwa yanaondolewa.

Maudhui yaliyokatazwa

16.-(1) Mtu hataruhisiwa kuchapisha maudhui yoyote yaliyokatazwa kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu.

(2) Mtu hatatoa, hatamiliki au kusambaza teknolojia, programu, kifaa au kitu kingine chochote kinachohusiana, kinachoruhusu au kusaidia watumiaji kupata maudhui yaliyokatazwa.

Kutoa taarifa

17.-(1) Mamlaka au mtu yeyote aliyeajiriwa na Mamlaka hatatoa taarifa yoyote iliyopokelewa au kupatikana wakati wa utekelezaji wa mamlaka yake au majukumu yake chini ya masharti ya Kanuni hizi, isipokuwa pale ambapo taarifa hiyo inahitajika na mamlaka zinazohusika kulingana na sheria.

(2) Bila kujali kanuni ndogo ya (1), mtu aliyeidhinishwa kutekeleza maagizo au anayesaidia kutekeleza maagizo hayo na kupata uelewa wa taarifa yoyote,

hatatumia au kutoa taarifa hiyo kwa mtu mwingine isipokuwa kama matumizi au utoaji wa taarifa hiyo ni muhimu kwa utekelezaji sahihi wa majukumu ya kiofisi kwa mtu aliyeidhinishwa.

Kumlinda mtoto

18. Mtu anayetoa, aliye na uwezo wa kupata, anayehodhi, anayetumia maudhui mtandaoni au anayeendesha huduma za intaneti atapaswa kuchukua hatua zote stahiki kuhakikisha kwamba:
(a) watoto hawajisajili, hawapati au kuchangia maudhui yaliyokatazwa; na
(b) watumiaji wanawekewa utaratibu wa kuchuja maudhui na usimamizi wa wazazi.

Uwezo wa Mamlaka

19. Katika kutekeleza majukumu yake ya udhibiti mtandaoni, Mamlaka itakuwa na uwezo ufuatao:
(a) kutoa leseni na kuwa na rejesta ya watoa huduma za maudhui mtandaoni;
(b) kuchukua hatua dhidi ya asiyezingatia Kanuni hizi, ikijumuisha kuagiza kuondolewa au kuzuia upatikanaji wa maudhui yaliyokatazwa; na
(c) kuhamasisha umma kuhusu matumizi salama ya maudhui mtandaoni.

Kushughulikia malalamiko

20.-(1) Mtu anaweza kuwasilisha malalamiko kwa mtoa huduma za maudhui mtandaoni kutokana na jambo lolote linahusiana na maudhui yaliyokatazwa na mmiliki wa leseni atatakiwa, kushughulikia malalamiko hayo ndani ya saa kumi na mbili.

(2) Endapo mtoa huduma za maudhui mtandaoni atashindwa kushughulikia malalamiko kwa muda uliowekwa, upande usioridhika unaweza kupeleka malalamiko kwa Mamlaka ndani ya siku thelathini tangu tarehe ya kuwasilisha malalamiko.

TS.Na. 203 la 2018

(3) Mamlaka itashughulikia malalamiko yaliyowasilishwa kwake chini ya kanuni ndogo ya (2) kwa mujibu wa Kanuni za Utaratibu wa Kuendesha Kamati ya Maudhui.

(4) Mtu asiyeridhishwa na uamuzi wa Mamlaka anaweza kukata rufaa kwenye Baraza la Haki la Ushindani.

Adhabu

21.-(1) Mtu anayekiuka masharti ya Kanuni hizi anatenda kosa na, atakapopatikana na hatia, pale ambapo

hakuna adhabu maalumu iliyoainishwa, atatozwa faini isiyopungua shilingi milioni tano au kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi kumi na miwili au vyote.

(2) Endapo ukiukwaji chini ya Kanuni hizi unafanywa na mmiliki wa leseni, Mamlaka inaweza kumpeleka kwenye Kamati ya Maudhui.

(3) Kamati ya Maudhui inaweza, baada ya uamuzi na kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), kuchukua moja au zaidi ya hatua zifuatazo:

(a) kutoa onyo kwa mmiliki wa leseni;
(b) kumtaka mmiliki wa leseni kuomba radhi kwa umma na kwa mwathiriwa wa maudhui yanayolalamikiwa;
(c) kuagiza kuondolewa kwa maudhui; au
(d) kutoza faini kwa mujibu wa Sheria.

Kufutwa kwa Tangazo la Serikali Na. 133 ya 2018

22. Kanuni za Mawasiliano za Kielektroniki na Posta (Maudhui Mtandaoni) za Mwaka 2018 zinafutwa.

## MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
IMETHIBITISHWA NA ISO 9001:2015

MAOMBI YA LESENI YA KUTOA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI

A: Aina ya Usajili unaouomba (Tafadhali weka alama ya vema)

1. Redio Mtandaoni ☐
2. Televisheni Mtandaoni ☐
3. Blogu Mtandaoni ☐
4. Huduma nyingine Mtandaoni ☐

B: Jina la redio /televisheni/blogu/huduma nyingine mtandaoni
……………………………………………………………
……………………………………………………………

C: Maelezo ya Mwombaji

1. Jina la mwombaji:……………………………….........................
Namba y simu:…………………………………………………………..
Namba ya kitambulisho cha Taifa.
……………………………………………………………
Baruapepe: …………………………………Tovuti..........…………….
Anwani ya Makazi………………………………………………………….
Mji/Jiji………………… Mtaa……..……… Na. ya Kitalu………………
Msimbo…………………………….

2. Majina ya wenye hisa na hisa zao:

*Tangazo la Serikali Na.913 (Linaendelea.)*

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

3. Hisa za mtaji wa Kampuni:
……………………………………………………………………………….
………………………………………………………………………………

4. Uraia wa waombaji wenye hisa/wakurugenzi (pamoja na namba za pasipoti na za Kitambulisho cha Taifa)

…………………………………………………………………………………………………
…
……………………………………………………………………………………………...…
…….
…………………………………………………………………………………………………
………

5. Namba ya Mlipakodi na Cheti Safi cha Kodi
……………………………………………………………………………….

6. Aina za leseni zinazoombwa:
   - Habari na Matukio ☐
   - Burudani ☐
   - Elimu/Dini ☐
   - Utangazaji sambamba ☐

7. Makadirio ya gharama za uwekezaji
………………………………………………………………………

8. Sifa za wafanyakazi
………………………………………………………………………

9. Programu za mafunzo ya wafanyakazi (ambatisha kama ipo)
……………………………………………………………………….

10. Tarehe inayotarajiwa ya kuanza kutoa huduma
……………………………………………………………………

11. Saa za huduma ……………………………………………

12. Ufafanuzi kama ni kwa ajili ya kupata faida au kutopata faida
…………………………………………………………………….

13. Mipango ya baadaye …………………………………………………

14. Maelezo mengine yoyote yanayofaa
…………………………………………………………………….

15. Uthibitisho:
Mimi/ Sisi………………………. tunathibitisha kwamba maudhui ya maombi haya na yote niliyoyaeleza humu ni ya ukweli na sahihi.

Saini ya mtu aliyeidhinishwa na mhuri wa ofisi.

Jina ……………………………..
Saini…………………………
Cheo…………………………..
Tarehe………………………………

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 6(1))*

ADA ZA HUDUMA ZA MAUDHUI MTANDAONI

| NA. | AINA YA LESENI | | ADA ZA MAOMBI (SH) | ADA ZA MWANZO (SH) | ADA ZA MWAKA(SH) | ADA ZA KUHUISHA (SH) | MUDA WA LESENI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Huduma za maudhui mtandaoni | Habari na matukio | 100,000 | 1,000,000 | 1,000,000 | 1,000,000 | Miaka 3 |
| | | Burudani | 100,000 | 500,000 | 500,000 | 500,000 | Miaka 3 |
| | | Elimu au Dini | 100,000 | 500,000 | 500,000 | 500,000 | Miaka 3 |
| | | | | | | | |
| 2. | Leseni ya televisheni ya utangazaji sambamba (maudhui katika mkondo wa intaneti) | | 50,000 | 200,000 | 200,000 | 200,000 | Miaka 3 |
| | | | | | | | |
| 3. | Leseni ya redio ya utangazaji sambamba(maudhui katika mkondo) | | 50,000 | 200,000 | 200,000 | 200,000 | Miaka 3 |

JEDWALI
LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

MAUDHUI YALIYOKATAZWA

Lolote kati ya yafuatayo ni maudhui yaliyokatazwa kwa madhumuni ya Kanuni hizi:

1. Ngono na matendo yasiyo na staha
   (a) maudhui yanayohamasisha, stawisha au kuwezesha uchapishaji au ubadilishanaji wa picha za ngono za watoto, picha halisi za ngono, vitendo dhahiri vya ngono, utupu na kinyume chake, isipokuwa kwa mandhari inayohusiana na iliyoidhinishwa na chombo kinachowajibika na upangaji wa madaraja ya filamu na uthibitisho;
   (b) kuhamasisha, kustawisha au kuwezesha kuchapisha au kubadilishana maudhui yanayohusu ushoga, uzinzi, ukahaba, uhalifu wa ngono, ubakaji au jaribio la ubakaji au ukatili wa kingono;
   (c) maudhui yanayohamasisha, kusaidia au kustawisha desturi au uuzaji wa bidhaa za ngono au zisizo na maadili kama vile filamu, picha, michoro, vitabu, hadithi, michezo ya ngono, madoli na vingine vinavyohusiana.

2. Uhuru Binafsi na Kuheshimu Utu
   (a) maudhui yanayoiga au kudai hadhi ya wengine kwa madhumuni ya ulaghai;
   (b) maudhui yanayotusi, kukashifu watu wengine au kufichua habari, picha au maoni yanayohusu uhuru binafsi wa mtu, au kuchapisha taarifa binafsi bila kujali kama taarifa hizo ni za kweli na iwapo uchapishaji wake unaweza kumuumiza mtu huyo;
   (c) maudhui yanayohamasisha au kustawisha udukuaji wa simu, upelelezi, wizi wa data, ufuatiliaji, kurekodi data au kunasa mawasiliano au mazungumzo bila ridhaa; na
   (d) maudhui yanayostawisha, kuhamasisha au kuchochea desturi za ushirikina, uchawi au ulozi.

3. Usalama wa Umma, Vurugu na Amani ya Taifa

(a) maudhui dhidi ya taifa na amani kwa umma ikijumuisha maudhui yanayolenga kusambaza taarifa, habari, maelezo au taarifa zisizokuwa na ukweli kwa madhumuni ya kukejeli, kudharau, kuharibu sifa, ufahari au hadhi ya Jamhuri ya Muungano, bendera ya Jamhuri ya Muungano, wimbo wa taifa au alama za Jamhuri ya Muungano, wimbo wa taifa au nembo zake;
(b) maudhui yanayovutia au kuhamasisha, kustawisha au kuchochea kutokuzingatia sheria na kanuni;
(c) maudhui yanayojihusisha kupanga, kuandaa, kuhamasisha au kuitisha maandamano, mikusanyiko au vitu vinavyoweza kuleta uvunjifu wa amani;
(d) maudhui yanayoweza kutishia usalama wa Jamhuri ya Muungano au kuhatarisha umma;
(e) maudhui yanayojumuisha habari za mawasiliano rasmi ya siri au masuala ya kijeshi;
(f) maudhui ambayo yanaweza kudhuru fedha ya taifa au kusababisha mkanganyiko juu ya hali ya uchumi nchini;
(g) maudhui ambayo yanachochea, yanahamasisha au yanawezesha kufanyika kwa uhalifu dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au raia wake;
(h) maudhui ambayo yanaweza kutishia utulivu wa Jamhuri ya Muungano au usalama wake, umoja au kudhuru umoja wa taifa au amani ya jamii;
(i) maudhui yanayoonyesha vurugu, ikiwa ni kwa uhalisia, maneno au kisaikolojia, yanayoweza kuvuruga, kuamsha na kuathiri watazamaji na kusababisha hofu miongoni mwa hadhira au kuhamasisha kuiga;
(j) maudhui yanayoonyesha vitendo vya udhalimu na mateso, picha za majeruhi wa kutisha na udhalimu na zenye damu au mandhari ya watu waliofanyiwa mauaji;
(k) maudhui yanayokera, kuchochea uharibifu au uovu, kuhamasisha au kuchochea uhalifu au kusababisha uvunjifu wa amani au kutishia amani ya taifa au ustawi wa umma na usalama;
(l) maudhui yanayohamasisha propaganda za chuki au kukuza mauaji ya kimbari au chuki dhidi ya kikundi kinachotambulika;
(m) maudhui yanayostawisha au kupendelea kile ambacho kingeleta uasi, chuki au ubaguzi wa rangi, ukabila au kudhuru umoja wa kitaifa au amani ya kijamii au kuvuruga utaratibu au maadili ya umma.

4. Vitendo vya Jinai na Biashara Haramu

(a) maudhui yanayohamasisha, yanayostawisha au kuwezesha matumizi ya dawa haramu, vitendo vya jinai na maarifa yanayohusisha maudhui yanayovutia, yanayostawisha au kutoa taarifa kuhusu jinsi ya kutenda jinai au uhalifu au kuchangia au kuwezesha utekelezaji au kusaidia matukio kama wizi, ulaghai, unyan'ganyi, kughushi, udanganyifu, uuaji, kujiua, usaliti, vitisho, ubakaji, utapeli wa kibiashara na kuvunja mali za wengine, utekaji nyara, ukwepaji wa sheria, utakatishaji fedha, maudhui yanayohamasisha magendo na jinai nyingine zinazoadhibiwa na sheria;

(b) maudhui yanayostawisha au kuchangia uuzaji wa dawa na dutu zinazoathiri akili na namna ya kutumia au kutengeneza vitu hivyo au kupata dawa au kuwezesha usambazaji katika mazingira ambayo hayajaidhinishwa kisheria;
(c) maudhui yanayohamasisha, kustawisha au kuwezesha biashara katika bidhaa zilizokatazwa au kuzuiwa, bidhaa au huduma ndani ya Jamhuri ya Muungano, zinazohusisha dawa haramu, ukahaba au bidhaa zinazohitaji leseni kutoka mamlaka yenye uwezo na ambazo zinazofanyiwa promosheni au kusambazwa bila idhini kutoka kwa mamlaka yenye uwezo;
(d) maudhui ambayo yanaendeleza kamari na shughuli kama hizo kama vile kubashiri na bahati nasibu na zile zinazohusiana na shughuli za kamari za kielektroniki;
(e) maudhui yanayohamisisha, kustawisha au kuwezesha makundi ya kigaidi au kikundi chochote haramu, chama, shirika au chombo;
(f) maudhui yanayochapisha aina ya kutengeneza risasi au vifaa vinavyolipuka au vifaa vingine vyovyote vinavyotumika kwenye matendo ya kigaidi.

5. Afya na Usalama wa Umma
(a) maudhui yanayohusu uanzishwaji wa vituo vya afya, dawa na utengenezaji wa dawa kinyume cha sheria;
(b) maudhui yanayojumuisha matangazo ya afya kinyume na maazimio ya Baraza la Mawaziri kuhusu matangazo ya afya;
(c) maudhui yanayotumika kufanya promosheni au biashara za dawa ambazo zimetolewa kinyume cha maagizo ya kutoa dawa hizo na bila kuuliza cheti cha utabibu;
(d) maudhui ambayo yanahamasisha dawa au bidhaa za dawa ambazo zimekatazwa au hazina leseni zikijumuisha virutubisho vya lishe, kupunguza uzito, uzito kuongezeka na vipodozi vya vidonge na krimu zisizo na leseni.

6. Ulindaji wa Haki za Milki ya Ubunifu
(a) maudhui yanayominya haki za milki ya ubunifu kama vile kutoa na kuchapisha filamu, picha, michoro, vitabu, michezo na programu za kielektroniki, vituo vya televisheni na redio zilizosimbwa na haki nyingine za milki ya ubunifu bila idhini kutoka kwa mmiliki wa haki;
(b) maudhui ambayo yanatoa taarifa, nyenzo na njia zinazokusudiwa kuminya haki za milki ya ubunifu na kupenyeza njia za ulindaji zinazotumiwa kulinda haki hizo kama vile kusimbua filamu na vituo vya televisheni vilivyosimbwa na uendeshaji wa disketi za kimagneti zilizonakiliwa na programu na michezo ya kielektroniki iliyonakiliwa na upunguzaji nguvu wa mifumo ya ulindaji iliyoundwa maalumu kwa ajili ya kuzuia uharamia;

7. Kuheshimu Dini na Imani ya Mtu

(a) maudhui ambayo yanayojumuisha au kuhamasisha kukera, kukashifu, kutukana, kubeza au kukiuka dini au ibada yake yoyote, takatifu au vitabu vya kimungu, au kuingiliwa uhuru wa mtu wa dini kwa vurugu au vitisho;
(b) maudhui yanayohamasisha, kustawisha au kuwezesha uchochezi au kejeli, chuki dhidi ya imani ya dini fulani au usemi unaohamasisha, kustawisha au kuwezesha kudhalilishwa kwa dini au uasi;
(c) maudhui ambayo yataweka aina yoyote ya ubaguzi na kuchochea matamshi ya chuki au kuchochea chuki za kikabila au kidini kwa nia ya kuchochea chuki ya watu au vikundi;
(d) maudhui ambayo hutumia dini kumfanya mtu binafsi au vikundi kutokuamini dini au kutokuwa na imani kwa kutumia moja ya njia ya kujieleza au kutumia njia yoyote ili kufikia maslahi maalumu au malengo haramu;

8. Taarifa za Umma ambazo zinaweza kusababisha uharibufu na machafuko kwa umma
(a) maudhui ambayo yanastawishi, yanatetea, yanahimiza au yanaweka wazi maelekezo na mwongozo wa shughuli haramu kama vile utengenezaji wa bomu, uzalishaji wa dawa haramu au bidhaa bandia;
(b) kusambaza au kutoa taarifa kuhusu uwezekano wa mashambulio ya kigaidi, ukame, utabiri wa hali ya hewa au kutokea kwa majanga ya asili bila idhini ya mamlaka husika;
(c) maudhui yenye taarifa zinazohusiana na kutokea kwa mlipuko wa magonjwa hatarishi au ya kuambukiza nchini au sehemu nyingine yoyote bila idhini ya mamlaka husika;
(d) kusambaza au kutoa taarifa kuhusu uhamasishaji wa dawa za matibabu na bidhaa za jumla za matibabu ambazo hazijaidhinishwa na mamlaka husika.

9. Utumiaji wa lugha chafu na maneno ya dharau
Maudhui yanayotumia lugha chafu, kama vile lugha ya dharau au maneno ya matusi ambayo yanachukuliwa kumchukiza mtu au kikundi cha watu, maneno machafu ya rejea, katika lugha yoyote inayotumika sana katika Jamhuri ya Muungano, ambayo yanachukuliwa kuwa ya uchafu au unajisi ikijimuisha rejea chafu ya kujamiana, viungo vya siri na hotuba ya chuki.

10. Maudhui ya Uongo, yasiyo ya ukweli na yanayopotosha
Maudhui ambayo ni ya uongo, yasiyo ya ukweli na yanayopotosha au ambayo yanaweza kupotosha au kudanganya umma isipokuwa pale ambapo imeelezwa kwa ufasaha kwamba maudhui ni ya kejeli, ubishi au uongo; na pale ambapo imetanguliwa na maelezo kwamba maudhui siyo ya kweli.

Dodoma, HARRISON G. MWAKYEMBE
............................, 2020 *Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo*